JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE

TANGAZO LA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UONGOZI NA MAADILI KWA MWAKA 2022

Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (The Mwalimu Nyerere Memorial AcademyMNMA) kinakaribisha maombi ya kujiunga na Mafunzo ya Uongozi, Maadili na Utawala Bora kwa mwaka 2022. Mafunzo haya hutolewa kila mwaka katika makundi mablimbali ambapo kila kundi lina fursa ya kuhudhuria Mafunzo haya mara moja kati ya nafasi mbili zinazotolewa kwa mwaka. Hivyo, Makundi ya Viongozi na watumishi mbalimbali wa serikalini na taasisi binafsi wanayo nafasi ya kuchagua muda ulio bora kwao na mahali ambapo kozi itatolewa illi kuweza kuhudhuria Mafunzo haya. Mpango huu wa Mafunzo ni wa mwaka mzima na yatafanyika katika kampasi mbili za Chuo Cha KumbuKumbu ya Mwalimu Nyerere yaani, Kampasi ya Kivukoni, Kampasi ya Karume Unguja na Kampasi ya Karume Tawi la Pemba (chakechake) ambapo mshiriki atachagua sehemu moja kati ya tatu zilizo orodheswa ili kuweza kushiriki Mafunzo haya. Washiriki watachagua awamu moja tu kati ya mbili zinazotolewa kwa mwaka kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapo chini.

Lengo

Lengo la Mafunzo haya ni kuwajengea uwezo washiriki katika stadi za Uongozi, Maadili na utawa bora na kuwajenga katika misingi imara ya Uongozi bora, uwajibikaji na uzalendo katika taasisi zao za Umma na binafsi kwa manufaa ya taifa la Tanzania.

Walengwa

Viongozi mbalimbali wa serikali, taasisi za serikali na binafsi pamoja na makundi mengine ya watu wanaofanya kazi katika nafasi mbalimbali za Uongozi na wote wenye nia ya kuwa Viongozi katika taasisi za umma na binafsi. Walengwa watatunukiwa cheti baada ya Mafunzo.

Ada ya Mafunzo

Gharama ya Mafunzo haya ni TZS 500,000/ ambayo italipwa kabla ya Mafunzo kuanza. Baada ya malipo, fedha haitaweza kurejeshwa. Malipo yote yatafanyika kwa kutumia control number atakayopewa mwombaji ili kuweza kufanya malipo kwaajili ya kushiriki mafunzo haya.

Jinsi ya kutuma maombi

Maombi kwa ajili ya kuhudhuria Mafunzo haya yako wazi kuanzia sasa.

Mwombaji atatuma maombi yake kwa njia ya mtandao kwa kujaza fomu iliyokatika tovuti ya Chuo ambayo ni: www.mnma.ac.tz.

Mwisho wa kutuma maombi kwa ajili ya Mafunzo haya itakuwa ni wiki moja kabla ya tarehe husika ya kuanza kwa mafunzo.

Mawasiliano

No	**Mahali Mafunzo yatakapotolewa**	**Afisa Mawasiliano**	**Simu**
1.	Kampasi ya Karume Tawi la Pemba - Zanzibar	Mohamed Mkangara	0655108108
2.	Kampasi ya Karume - Zanzibar	Jumanne Kassim Katimle	0752122224
3.	Kampasi ya Kivukoni – Dar es Salaam	Vivian Kapilima	0714034425

Kwa mawasiliano zaidi kuhusu programu hii maalumu ya Uongozi na Maadili unaweza kuwasiliana na Dr. Phillip D. Daninga, Mratibu wa Mafunzo ya Uongozi, Maadili na Utawala Bora kupitia namba ya simu ya mkononi 255(22)2820041/47 au +255675337734: email: kibweta@mnma.ac.tz au rector@mnma.ac.tz

Imetolewa na:

Mkuu wa Chuo
Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE (THE MWALIMU NYERERE MEMORIAL ACADEMY - MNMA)						
PROGRAMU YA MAFUNZO YA UONGOZI, MAADILI NA UTAWALA BORA KWA MWAKA 2022						
Na.	**Kundi la Washiriki**	**Washiriki**	**Awamu ya Kwanza**	**Tarehe za Mafunzo Kwa Mwaka**		**Mahali**
1	Watumishi wa Serikali na Taasisi Binafsi	Watumishi wa serikali, Wakuu na watumishi wa taasisi binafsi	Februari na Julai	(21/02 – 25/2/2022)	Julai (18 - 22, 2022)	MNMA Kampasi ya Kivukoni –DSM, Zanzibar (Kampasi ya Karume, Tawi la Pemba)
2	Tawala za Wilaya	Wakuu wa shule na Idara, shule za Msingi na Sekondari	Februari na Agosti	(21/02 – 25/2/2022)	Agosti (1 - 5, 2022)	MNMA Kampasi ya Kivukoni –DSM, Zanzibar (Kampasi ya Karume, Tawi la Pemba)
		Ma Afisa Tawala wa Wilaya – RAS; Wakuu wa Idara na Vitengo Halmashauri na manispaa	Februari na Agosti	Februari (21/2/2022 - 25/2/ 2022)	Agosti (8 - 12, 2022)	MNMA Kampasi ya Kivukoni –DSM, Zanzibar (Kampasi ya Karume, Tawi la Pemba)
					Agosti (15 - 19, 2022)	MNMA Kampasi ya Kivukoni –DSM, Zanzibar (Kampasi ya Karume, Tawi la Pemba)
		Wakurugenzi wa wilaya na manispaa	Februari na Agosti	Februari (21/2/2022 - 25/2/ 2022)	Agosti (22 - 26, 2022)	MNMA Kampasi ya Kivukoni –DSM, Zanzibar (Kampasi ya Karume, Tawi la Pemba)

3	Serikali za Mitaa	Watendaji Kata na vijiji	Machi na Septemba	Machi (14 - 18, 2022)	Septemba (19 - 23, 2022)	MNMA Kampasi ya Kivukoni –DSM, Zanzibar (Kampasi ya Karume, Tawi la Pemba)
4	Tawala za Mikoa	MaAfisa Tawala wa Mikoa - RAS	Aprili na Oktoba	Aprili (25 - 29,2020)	Oktoba (10 - 14, 2022)	MNMA Kampasi ya Kivukoni –DSM, Zanzibar (Kampasi ya Karume, Tawi la Pemba)
5	Taasisi za Elimu ya Juu	Wakuu wa vyuo na vitivo	Mei na Novemba	Mei (16 - 20, 2022)	Novemba (13 - 18, 2022)	MNMA Kampasi ya Kivukoni –DSM, Zanzibar (Kampasi ya Karume, Tawi la Pemba)
		Wakuu wa Idara na Vitengo	Juni na Desemba	Juni (13 - 17, 2022)	Desemba (12 - 16,2022)	MNMA Kampasi ya Kivukoni –DSM, Zanzibar (Kampasi ya Karume, Tawi la Pemba)

Kujiunga na mafunzo haya mwombaji anatakiwa kujaza fomu iiyopo kwenye link hii:

https://https://www.mnma.ac.tz/kibweta/apply